




# Zege imelala?

## Maoni ya Watanzania kuhusu kukwama kwa mchakato wa marekebisho ya katiba

## 1. Utangulizi

Mchakato wa kurekebisha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulianza baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Vyama viwili vikuu vya upinzani nchini, CHADEMA na CUF ndivyo vilivyoanzisha vugu vugu ya kudai katiba mpya. Umuhimu wa katiba mpya ndio ulikuwa msingi wa kampeni za uchaguzi za vyama hivyo. Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliitikia wito huo kwa kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Katiba. Hata hivyo mchakato huo ulisimama mwaka 2015, kupisha uchaguzi mkuu wa 2015, na haujaendelea tena tangu kipindi hicho.

Mchakato wa marekebisho ya katiba ulipitia awamu kuu tatu. Awamu ya kwanza ilikuwa ya kuundwa kwa Tume ya marekebisho ya Katiba. Hii iliundwa chini ya uongozi wa Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Sinde Warioba na Tume hii ilisafiri nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi kuhusu muundo wa katiba mpya na ikachapisha rasimu yake ya kwanza baada ya kupata maoni ya wananchi. Rasimu hii ilijulikana kama "rasimu ya Warioba" na ilichapishwa mwezi Disemba mwaka 2013. Miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa katika rasimu hii ni kubadilisha muundo wa sasa wa serikali mbili (Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibari) na kuanzisha muundo wa serikali tatu (Serikali ya Muungano, Serikali ya Tanzania Bara, Serikali ya Zanzibari).

Katika awamu ya pili, Bunge Maalumu la Katiba, ambalo lilijumuisha wanachama wote wa Bunge la Muungano pamoja na wanachama wote wa Baraza la Wawakilishi kutoka Zanzibar, pamoja na wanachama walioteuliwa kutoka vyama vya siasa na asasi za kiraia, walikutana mwaka 2014 kupitia rasimu hiyo ya katiba. Mabadiliko muhimu yalifanyika kwenye rasimu ya Warioba chini ya uongozi wa Samwel Sitta aliyekuwa

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
+255 22 266 4301 | info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti

JUKWAA LA KATIBA TANZANIA & Twaweza ni sisi

mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba na Andrew Chenge aliyekuwa mwenyekiti wa kamati ya uandishi wa katiba mpya. Suala la kubadili muundo wa serikali mbili kwenda muundo wa serikali tatu liliondolewa.

Rasimu hii mpya, ilijulikana rasmi kama "Katiba inayopendekezwa" japo ilipata umaarufu kwa kujulikana kama "rasimu ya Chenge". Bunge Maalumu la Katiba lilipitisha rasimu hii mwezi Oktoba mwaka 2014, pasipo kujali kujiondoa kwa wajumbe wa bunge la katiba waliounda umoja wao uliojulikana kama, Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Umoja huu uliundwa pale wajumbe wa bunge la katiba kutoka vyama vya upinzani na baadhi ya wawakilishi wa asasi za kiraia, walipoona kuwa chama tawala (CCM) kilikuwa kikitumia wingi wa wajumbe wake kwenye bunge hilo kuhujumu vipengele vilivyopendekezwa kwenye rasimu ya tume iliyoongozwa na jaji Warioba.

Katiba iliyopendekezwa ilitakiwa kupigiwa kura ya maoni na wananchi mwaka 2015, lakini jambo hilo halikufanikiwa. Changamoto za uandikishaji wa wapiga kura, pamoja na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba mwaka 2015, vilichangia zoezi la upigaji kura wa Katiba kuahirishwa. Hata hivyo, ilani ya uchaguzi ya CCM ilionesha kuunga mkono katiba iliyopendekezwa na kuahidi kuongoza vema zoezi la kumalizia mchakato mzima wa katiba mpya. Lakini mpaka sasa, serikali ya awamu ya tano, haijatimiza ahadi yake ya kuamsha mchakato huu muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu; jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa sintofahamu ya hatma ya suala zima la katiba mpya.

Muhtasari huu umebeba maoni ya wananchi juu ya mchakato wa mabadiliko ya katiba na namna unavyoweza kuendelezwa. Ni kwa kiasi gani wananchi waliufahamu na kuuelewa mchakato huu? Je, walitambua umuhimu wa ushiriki wao katika zoezi la kukusanya maoni? Je, wanakubaliana na mabadiliko yaliyofanyika kwenye katiba katika kila hatua? Je, wanakubaliana na kitendo cha UKAWA kususia mchakato huo? Je, wangependa mchakato huu uanze tena, na kama ndivyo, ufanyike kwa utaratibu gani?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* ambao huratibiwa na taasisi ya Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi; na wenye uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Zanzibari haihusiki kwenye utafiti huu. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,745 kutoka awamu ya 20 ya kundi la pili la *Sauti za Wananchi*, zilizokusanywa kati ya tarehe 27 Juni na 14 Julai, 2017.

Matokeo muhimu ni:

- Karibu wananchi wote wamesikia kuhusu katiba, lakini ni mwananchi 1 tu kati ya 3 anayeweza kueleza katiba ni nini.
- Wananchi 7 kati ya 10 wanafahamu kuhusu mchakato wa mabadiliko ya katiba.
- Mwananchi 1 kati ya 5 alishiriki katika kutoa maoni yake kwenye zoezi lililoratibiwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.
- Uelewa wa katiba na mchakato wa mabadiliko, na pia ushiriki kwenye mchakato huo ni

mdogo zaidi miongoni mwa wanawake kuliko wanaume.


- Wananchi 2 kati ya 3 wanasema mchakato huo haukuruhusu maoni ya wananchi kuingizwa kwenye katiba
- Wananchi wanapinga mabadiliko mengi yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba, ikiwemo uamuzi wa kuondoa mamlaka ya bunge kupitisha mawaziri walioteuliwa.
- Miongoni mwa wananchi wa Tanzania Bara, muundo wa serikali unaokubalika zaidi ni wa serikali mbili.
- Mwananchi 1 kati ya 4 anaunga mkono UKAWA kulisusia Bunge Maalumu la Katiba na kuugomea mchakato wa mabadiliko ya katiba.
- Chaguo la wananchi la kurudia mchakato wa mabadiliko ya katiba ni kuanza upya kabisa na kuunda tume mpya.
- Kama mchakato utaanzishwa upya, wananchi wangependa ukurasa mpya kabisa ufunguliwe au uanzie kwenye rasimu ya Warioba.
- Wananchi 2 kati ya 3 wanasema Tanzania inahitaji katiba mpya na wananchi 3 kati ya 10 wanasema hili litafanikiwa ndani ya miaka mitatu ijayo.

# 2. Mambo tisa kuhusu maoni ya wananchi juu ya katiba

## Jambo la 1: Wananchi wengi wamesikia kuhusu katiba lakini ni mwananchi 1 tu kati ya 3 anayeweza kueleza maana ya katiba

Asilimia 93 ya Watanzania wameshawahi kusikia kuhusu katiba, lakini kati ya hao, asilimia 58 hawafahamu katiba ni nini. Asilimia 22 wanasema katiba ni mkusanyiko wa kanuni zinazotumika kuongoza nchi na asilimia 12 wanasema kuwa katiba ni azimio la kisheria linalotumika kuongoza nchi. Ni asilimia ndogo tu (asilimia 1) wanaosema ni azimio la haki za wananchi. Maelezo yote matatu yanaweza kuwa sahihi, kwa kuwa yanaeleza kazi moja ama zaidi za katiba ya nchi.

**Jambo la 1: Unaposikia neno Katiba, lina maana gani kwako?**[1]




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)


*Idadi ya wahijowa wote =1745*

1 Jumla ya asilimia zote zinaweza zisifike 100% kutokana na makadirio

Uelewa kuhusu maana ya katiba ni mkubwa miongoni mwa wenye elimu ya sekondari na elimu ya juu (asilimia 49) kuliko wale ambao hawajahitimu elimu ya msingi (asilimia 22). Vilevile ni mkubwa miongoni mwa wananchi wenye umri zaidi ya miaka 50 (asilimia 45) kuliko wenye umri chini ya miaka 30 (asilimia 29), na miongoni mwa wananchi matajiri (asilimia 40) kuliko masikini (asilimia 28). Hata hivyo, suala lililojitokeza zaidi ni tofauti ya uelewa wa dhana hiyo kati ya wanaume na wanawake, asilimia 47 ya wanaume waliweza kueleza maana ya katiba, ukilinganisha na asilimia 22 ya wanawake (hii haijaoneshwa kwenye jedwali).

Asilimia 44 ya wananchi wanasema katiba iliyopo sasa inatekelezwa ipasavyo, na asilimia 46 wanasema inatekelezwa "kwa kiwango fulani." Ni kikundi kidogo tu (asilimia 4) kinachosema "haitekelezwi ipasavyo."

**Kielelezo cha 2: Ni kwa kiwango gani katiba iliyopo (1977) inatekelezwa ipasavyo nchini Tanzania?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)
*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Walipotakiwa kueleza sababu za tathmini waliyotoa, wengi waliosema katiba inatekelezwa ipasavyo walisema kuwa kwa maoni yao ni kwasababu sheria zinafuatwa (asilimia 22) au kutokana na kwamba uongozi ni mzuri (asilimia 12). Wengi kati ya wale waliosema "inatekelezwa kwa kiwango fulani" walieleza kuwa kuna baadhi ya vipengele vya katiba ambavyo havifuatwi (asilimia 15) au sheria kadhaa ambazo hazifuatwi (asilimia 12) (hii haijaoneshwa kwenye jedwali).

## Jambo la 2: Wananchi 7 kati ya 10 wanaufahamu mchakato wa mabadiliko ya katiba

Asilimia 71 ya wananchi wanafahamu kuwa serikali ya Tanzania ilianzisha mchakato wa mabadiliko ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uelewa wa mchakato huo ni mkubwa miongoni mwa wanaume (asilimia 81) ukilinganisha na wanawake (asilimia 61), miongoni mwa wenye umri wa miaka zaidi ya 50 (asilimia 81) kuliko wenye umri chini ya miaka 30 (asilimia 63). Na pia wale wenye elimu ya sekondari au elimu ya juu (asilimia 80) kuliko wale ambao hawajahitimu elimu ya msingi (asilimia 62). Ufahamu miongoni mwa wananchi matajiri na waishio maeneo ya mijini ni mkubwa, japokuwa utofauti huu ni mdogo.

**Kielelezo cha 3: Je, unafahamu kuwa serikali ilianzisha mchakato wa mabadiliko ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchukua nafasi ya Katiba ya Mwaka 1977?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* (Juni- Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Nusu ya wananchi (49%) wanafahamu juu ya mchakato wa kukusanya maoni uliofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya uongozi wa Jaji Warioba na mwananchi mmoja kati ya wanne (23%) wanafahamu kilichotokea baada ya kukamilika kwa kazi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Vile vile mwananchi mmoja kati ya watano (21%) wanafahamu kuwa vipengele vya "rasimu ya Warioba" viliondolewa na Bunge Maalumu la Katiba kupitia katiba inayopendekezwa au "rasimu ya Chenge."

**Kielelezo cha 4: Ufahamu kuhusu hatua muhimu na mabadiliko katika mchakato wa uundaji wa katiba mpya**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

## Jambo la 3: Mwananchi 1 kati ya 5 alishiriki kwenye mchakato wa kutoa maoni ulioendeshwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba

Mwananchi mmoja kati ya watano (18%) alishiriki kwa namna fulani katika mchakato wa kukusanya maoni wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Yafaa ifahamike kuwa Novemba mwaka 2013, 36% ya wananchi walieleza kuwa waliwasilisha maoni yao kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kupitia mikutano, barua, mitandao au ujumbe wa simu[2]. Mwananchi mmoja kati ya nane (12%) anasema alihudhuria mkutano wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, na idadi ndogo wanasema walihojiwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba (6%) au waliwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi (4%), kupitia ujumbe wa simu (3%) au kwa barua pepe ama mitandao ya kijamii (1%).

**Kielelezo cha 5: Mchakato wa mabadiliko ya katiba ulihusisha kukusanya maoni ya wananchi. Tafadhali niambie ulishiriki katika jambo lipi kati ya haya yafuatayo?**





**Chanzo takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

2 *Sauti za Wananchi* Kurasimu Sheria Mama ya Nchi, Novemba 2013, http://www.twaweza.org/go/sauti-katiba-kis

Wanaume wameonesha viwango vikubwa vya ushiriki kwenye mchakato wa kutoa maoni wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba (25%) kuliko wanawake (10%). Wenye umri zaidi ya miaka 50 (24%) walikuwa na uwezekano zaidi wa kushiriki kuliko wenye umri chini ya miaka 30 (13%). Tofauti katika viwango vya ushiriki kati ya makundi yenye uwezo mbalimbali ni ndogo, sawa na wananchi wenye viwango tofauti vya elimu na wale wanaoishi maeneo ya mijini na vijijini.

**Kielelezo cha 6: % ya walioshiriki angalau kwenye jambo moja katika mchakato wa uundaji wa katiba mpya**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)


*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

## Jambo la 4: Wananchi 2 kati ya 3 wanasema maoni ya wananchi hayajatokea kwenye rasimu ya katiba

Mwananchi mmoja kati ya watatu (33%) wanasema mchakato wa mabadiliko ya katiba ulihusisha kusikiliza na kuwakilisha maoni ya wananchi kwenye rasimu ya katiba iliyotengenezwa. Mwananchi mmoja kati ya wanne (23%) wanasema mchakato huo kwa kiasi kikubwa ulikuwa ni kuwapa wananchi taarifa kuliko kuruhusu wananchi kutoa maoni yao. Waliobaki (44%) waliona mchakato huo uliwapa fursa wananchi kutoa maoni yao, lakini hayakutumika kwenye rasimu ya katiba.

Imani kuwa mchakato mzima ulikuwa wa ushirikishwaji ni mkubwa miongoni mwa wananchi wasio na uwezo kuliko wale wenye uwezo.

**Kielelezo cha 7: Fikiria kuhusu mchakato wa uundaji wa katiba mpya nchini Tanzania, kauli ipi kati ya zifuatazo inaelezea vizuri namna mchakato huo ulivyofanyika nchini Tanzania?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Wananchi tisa kati ya kumi (91%) wanakubaliana na kauli kuwa “mchakato wa mabadiliko ya katiba na maudhui ya katiba ni muhimu” (haijaoneshwa kwenye jedwali). Kwa kuongezea, wananchi sita kati ya kumi (59%) wanasema Bunge Maalumu la Katiba liliwakilisha vema watanzania katika mchakato huo. Wananchi wanne kati ya kumi (38%) hawakubaliani na kauli hiyo (haijaoneshwa kwenye jedwali).

Pale walipoulizwa nani anapaswa kuongoza mchakato wa mabadiliko ya katiba, mwananchi mmoja kati ya watano (20%) anasema kuwa wananchi walipaswa kuongoza mchakato huo. Mwananchi mmoja kati ya kumi (11%) anasema hivyo ndivyo ilivyokuwa. Vilevile, nusu ya wananchi (49%) wanasema Rais ndiye aliyepaswa kuongoza mchakato huo, wakati wananchi wanne kati ya kumi (39%) wanasema Rais ndiye aliyeongoza mchakato huo. Inashangaza kuona kuwa 26% ya wananchi hawafahamu aliyeongoza mchakato mzima wa kupata katiba mpya.

**Kielelezo cha 8: Unadhani ni nani aliyeongoza mchakato wa mabadiliko ya katiba? Unadhani nani alipaswa kuongoza mchakato huo?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

## Jambo la 5: Wananchi hawakubaliani na mabadiliko mengi yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba

Wananchi hawakubaliani na mabadiliko mengi yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba chini ya mwenyekiti wa kamati ya uandishi wa katiba mpya, Andrew Chenge. Wananchi nane kati ya kumi (79%) hawakubaliani na kuondolewa kwa kifungu kinachotaka mawaziri kupitishwa ama kukataliwa kwa kura bungeni mara baada ya kuteuliwa na Rais. Wananchi wawili kati ya watatu (64%) hawakubalini na kuondolewa kwa kifungu cha wananchi kuwaondoa wabunge wao pale wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao.

Wananchi wengi pia hawakubaliani na uamuzi wa kuondoa kifungu kinachowakataza viongozi na watumishi wa umma kuwa na akaunti za benki nje ya nchi (54%) na kuondolewa kwa kipengele kinachoweka ukomo wa miaka 15 kwa mbunge.


Wananchi wamegawanyika nusu kwa nusu (48% - 45%) kuhusu Bunge Maalumu la Katiba kuondoa "uwazi na uwajibikaji" kwenye orodha ya tunu za taifa kwenye katiba.

Mabadiliko matatu yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba ambayo yanaungwa mkono na wananchi wengi ni uamuzi wa kuondoa usawa wa 50-50 wanaume na wanawake bungeni, kuondoa baadhi ya madaraka ya Rais na kuondoa pendekezo la mawaziri kuteuliwa kutoka nje ya bunge.

Kwa ujumla, wananchi waliokuwa na uelewa wa maana ya katiba walionesha uwezekano mdogo wakuunga mkono mabadiliko haya(takwimu hazijaoneshwa).

Kukubalika kwa marekebisho haya kumeonekana kuongezeka tangu kukamilishwa kwa kazi za Bunge la Katiba. Mwaka 2015, asilimia 47 waliunga mkono kuondolewa kwa kipengele cha kuteua mawaziri kutoka nje ya bunge, idadi hiyo imeongezeka hadi nasilimia 62 mwaka huu. Pamoja na hayo, kuondolewa kwa ukomo (wa miaka 15) wa mbunge kushika madaraka pia kunaungwa mkono zaidi (asilimia 26 hadi asilimia 45), na kuondolewa kwa uwazi na uwajibikaji kwenye orodha ya tunu za taifa kunakubalika zaida kutoka asilimia 21 hadi asilimia 48. Asilimia 34 wanaunga mkono kuondolewa kwa kifungu cha wananchi kuwaondoa madarakani wabunge wao wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao. Idadi hii ilikuwa asilimia 19 mwaka 2015. (Takwimu hizi hazijaoneshwa)

**Kielelezo cha 9: Ni kwa kiwango gani unakubaliana na mabadiliko yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

## Jambo la 6: Miongoni mwa watanzania Bara, muundo wa serikali unaokubalika zaidi ni wa serikali mbili unaotumika hivi sasa


Wananchi wanne kati ya kumi Tanzania Bara (42%) wanaona kuwa muundo uliopo wa serikali mbili ndio muundo sahihi zaidi kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuliko mifumo mingine iliyopendekezwa. Mwananchi mmoja kati ya nane (12%) wanasema muundo mzuri ni ule unaofanana na muundo wa sasa lakini Tanzania visiwani ipewe uhuru zaidi. Mwananchi mmoja kati ya sita (16%) wanachagua muundo wa serikali tatu, kama ulivyopendekezwa na

Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya Jaji Warioba, na mwananchi mmoja kati ya wanne (25%) wanapendelea wazo la muundo wa serikali moja.

Kwa Tanzania Bara, viwango hivi vimebadilika kidogo tangu utafiti ulipofanyika mwaka 2014. Uungaji mkono wa muundo wa serikali unaotumika hivi sasa umeongezeka kutoka 25% mpaka 42% na uungaji mkono wa muundo wa serikali tatu umeshuka, kutoka 22% mpaka 16%.

Ifahamike kuwa viwango vilivyooneshwa hapo juu vyote vinatoka Tanzania Bara, na pale ambapo utafiti unaofanana na huo ulipofanyika Zanzibar mwaka 2014, maoni ya wananchi yalikuwa tofauti na yale ya wananchi wa Tanzania Bara. Miongoni mwa wakazi wa Zanzibar, uungaji mkono wa muundo wa serikali unaotumika hivi sasa ni mdogo sana, ambapo ni mwananchi mmoja tu kati ya ishirini (5%) waliochagua chaguo hilo. Idadi kubwa ya wananchi waligawanyika kati ya muundo wa serikali tatu (46%) au muundo wa serikali mbili lakini ambao utatoa uhuru zaidi kwa Zanzibar kuliko ilivyo sasa.

**Kielelezo cha 10: Mapendekezo ya wananchi kuhusu muundo wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania****




* 2014: Mabadiliko yapi, kama yapo, ungependa kuona kwenye muungano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar? 2017: Muundo gani wa serikali ambao unadhani ni sahihi kwa Tanzania?

** Serikali mbili, uhuru kidogo kwa ZNZ hayakuorodheshwa kwenye orodha ya majibu katika tafiti za 2014

**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 1 Awamu ya 14 (Februari 2014) na Kundi la 2 Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017);

*Utafiti wa Wasemavyo Wazanzibari – Awamu ya 6, Februari 2014*


*Wahojiwa wote: 2017 - Idadi ya wahojiwa =1745; 2014*

*(Bara) - Idadi ya wahojiwa =1547; 2014*

*(Zanzibar) - Idadi ya wahojiwa = 445*

Vilevile, wananchi watatu kati ya wanne kutoka Tanzania Bara (72%) wanasema wanakubaliana na uamuzi wa Bunge Maalumu la Katiba wa kuendelea na muundo wa serikali mbili, badala ya kukubali muundo wa serikali tatu kama ulivyopendekezwa na Tume ya Mabadiliko ya katiba.

**Kielelezo cha 11: Kwa kiwango gani unakubaliana na uamuzi wa Bunge Maalumu la Katiba kuondoa muundo wa serikali tatu na kuendelea na serikali mbili**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)
*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

## Jambo la 7: Mwananchi mmoja kati ya wanne wanaunga mkono UKAWA kususia Bunge Maalumu la Katiba na kugomea mchakato wa kupitia katiba

Mwananchi mmoja kati ya wanne (23%) wanaunga mkono uamuzi wa muungano wa upinzani, UKAWA (Umoja wa Katiba ya Wananchi), kutoka nje ya Bunge Maalumu la Katiba na kugomea mchakato wa katiba uliokuwa umebaki. Mwananchi mmoja kati ya wanne (26%) hawafahamu kususiwa kwa mchakato wa katiba, huku nusu ya wananchi (48%) wakipinga kitendo kilichofanywa na UKAWA.

Idadi kubwa kidogo ya wananchi (56%) wanasema kutoka nje kwa UKAWA hakufanyi mchakato wa katiba kuwa batili, wakati wananchi wanne kati ya kumi (41%) wanasema kitendo hicho kinaondoa uhalali wa mchakato huo.

**Kielelezo cha 12: Maoni kuhusu UKAWA kususia/kutoka nje ya Bunge Maalumu la Katiba**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)
*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Hata hivyo, walipoulizwa kwa kutumia kauli ya jumla bila kutaja jina UKAWA, mtazamo ulibadilika. Idadi kubwa (56%) wanakubaliana na kauli kuwa “kama kikundi kikiamua kutoshiriki kwenye mchakato wa mabadiliko ya katiba, hufanya katiba kukosa uhalali miongoni mwa wananchi wote” (haijaoneshwa kwenye jedwali).

## Jambo la 8: Mwananchi mmoja kati ya wawili wanasema njia nzuri ya kufufua mchakato wa katiba ni kuanza upya kabisa na tume mpya

Karibu nusu ya wananchi (48%) wanasema kuwa njia nzuri ya kufufua mchakato wa mabadiliko ya katiba ni kuanza mchakato huo upya na tume mpya. Wananchi wawili kati ya kumi (18%) wanasema njia nzuri ni kwenda moja moja na kuipigia kura rasimu ya Warioba. Idadi ndogo (13%) wanasema njia sahihi ni kuipigia kura rasimu ya Chenge/katiba inayopendekezwa, wakati wananchi wachache sana wanasema mchakato uanze upya na Bunge jipya la Katiba (9%) au rasimu ipelekwe bungeni ili wabunge wafanyie kazi tolea jipya (6%). Wananchi waliokuwa na uelewa wa maana ya katiba walionesha kupendelea zaidi kufufua mchakato wa mabadiliko ya katiba kwa kupigia kura rasimu ya katiba ya Warioba; asilimia 25 ikilinganishwa na asilimia 18.

**Kielelezo cha 13: Ni njia gani nzuri ya kufufua mchakato wa mabadiliko ya katiba nchini Tanzania?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Walipoulizwa ni toleo gani la katiba litumike kama sehemu ya kuanzia majadiliano iwapo mchakato wa katiba utaanzishwa tena, wananchi wanne kati ya kumi (38%) wanasema tuanze "ukurasa mpya" na wananchi watatu kati ya kumi (31%) wanasema rasimu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba (rasimu ya Warioba) itumike. Mwananchi mmoja kati ya sita (16%) wanapendekeza mchakato uanzie kwenye katiba ya mwaka 1977 inayotumika hivi sasa na mwananchi mmoja kati ya kumi (11%) wanasema itumike katiba iliyopendekezwa na Bunge Maalumu la Katiba (toleo la Chenge). Wananchi waliokuwa na uelewa wa maana ya 'katiba' walionesha kupendelea zaidi kufufua mchakato wa mabadiliko kwa kurejea kwenye rasimu ya katiba ya Warioba na kuanza hapo (asilimia 43 ikilinganishwa na asilimia 31) kuliko kuanza na ukurasa mpya (asilimia 26 ikilinganishwa na asilimia 38.)

**Kielelezo cha 14: Kama mchakato wa mabadiliko ya katiba utaanzishwa tena, toleo gani la katiba litumike kama mahali pa kuanzia?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)


*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Idadi kubwa ya wananchi (56%) wanasema kuwa mchakato wowote utakaotumika kuandaa katiba mpya, uamuzi wa mwisho ufanywe na wananchi kupitia kura ya maoni. Mwananchi mmoja kati ya wanne (24%) wanasema kuwa maamuzi ya mwisho yafanywe na bunge (haijaoneshwa kwenye jedwali).

## Jambo la 9: Wananchi 2 kati ya 3 wanasema kuwa Tanzania inahitaji katiba mpya, wananchi 3 kati ya 10 wanasema katiba mpya itapatikana ndani ya miaka mitatu ijayo

Wananchi wawili kati ya watatu (67%) wanasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahitaji katiba mpya, ukilinganisha na mwananchi mmoja kati ya wanne (24%) ambao hawaoni umuhimu huo. Hata hivyo, wananchi wengi hawadhani kama hili linaweza kutokea hivi karibuni. Wananchi watatu kati ya kumi (30%) wanasema Tanzania itapata katiba mpya miaka mitatu ijayo, ukilinganisha na wananchi watano kati ya kumi (48%) ambao hawafikiri hivyo.

**Kielelezo cha 15: Je, unadhani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahitaji katiba mpya? Je, unadhani Tanzania itapata katiba mpya miaka mitatu ijayo?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 20 (Juni-Julai 2017)

*Idadi ya wahojiwa wote = 1,745*

Walipoulizwa kwa nini katiba mpya inahitajika, wananchi watatu kati ya kumi (31%) wanasema katiba ya mwaka 1977 ni ya zamani au imepitwa na wakati. Walipoulizwa kwa nini katiba mpya haitapatikana miaka mitatu ijayo, wananchi walitoa sababu mbalimbali, ikiwemo kuwa miaka

mitatu haitoshi (14%), kukosekana kwa muafaka kuhusu maudhui ya katiba (8%) na kukosekana kwa mwamko kwa upande wa serikali (8%) (haijaoneshwa kwenye jedwali).

# 3. Hitimisho

Muhtasari huu unatupa maelezo muhimu juu ya mitazamo ya wananchi kuhusu mchakato mzima wa mabadiliko ya katiba uliofanyika kati ya mwaka 2010 na 2015, na tathmini yao kuhusu jitihada hizo. Lakini maoni ya msingi zaidi ni yale ambayo yatatusaidia kusonga mbele. Je, tunajifunza nini? Je, wananchi wana hamu ya kuanza tena upya mchakato wa mabadiliko ya katiba? Na kama ndivyo, je, ufanyike vipi?

Tukitazama tulikotoka, matokeo muhimu ni yale yanayotoa maelekezo kwa yeyote anayewaza kuanza tena mchakato wa mabadiliko ya katiba nchini Tanzania. Hapa, vinajitokeza vitu vitatu. Kwanza, kiwango cha uelewa na ufahamu wa wananchi kuhusu mchakato wa mabadiliko ya katiba si kikubwa sana. Asilimia 93 ya wananchi wamesikia kuhusu katiba, lakini ni asilimia 35 tu waonaweza kueleza maana ya katiba kwa kujiamini, na robo ya wananchi hawafahamu kama mchakato wa mabadiliko ya katiba ulifanyika.

Pili, kuna changamoto kubwa katika kuhakikisha wananchi wote wanashirikishwa, hususani wanawake. Uelewa wa katiba, na uelewa wa mchakato mzima wa mabadiliko ya katiba, pamoja na ushiriki katika mchakato huo ni mdogo miongoni mwa wanawake kuliko wanaume. Kuna dalili pia kwamba vijana, wananchi masikini na wasiokuwa na elimu hawakuhusishwa ipasavyo.

Tatu, wananchi wana maoni tofauti kuhusu kujiondoa kwa UKAWA katika Bunge maalumu la Katiba. Idadi kubwa hawaungi mkono maamuzi ya UKAWA. Lakini walipoulizwa kwa kauli ya ujumla, bila ya kutaja jina UKAWA, idadi kubwa walisema kama kikundi fulani kikiamua kutoshiriki, matokeo yake mchakato mzima unakosa uhalali.

Maoni ya wananchi kuhusu maudhui ya katiba yanafaa kuzingatiwa. Mabadiliko mengi yaliyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba yanayoendana na uwajibikaji hayafahamiki. Kuna idadi kubwa ya wananchi wanaotofautiana na maamuzi ya kuondoa vifungu vilivyotaka bunge kupitisha mawaziri walioteuliwa na Rais na wapiga kura kuwavua madaraka wabunge walioshindwa kutekeleza majukumu yao. Vile vile idadi ndogo ya wananchi wanapinga kuondolewa kwa kipengele kinachokataza viongozi wakubwa wa serikali kumiliki akaunti za benki nje ya nchi na kuondolewa kwa kipengele kinachotaka ukomo wa ubunge uwe miaka 15.

Katika suala ambalo lilitawala mjadala na vichwa vya habari kuhusu katiba mpya – ni suala la muungano – muhtasari huu unabainisha muundo unaopendwa zaidi miongoni mwa wananchi wa Tanzania Bara ambao ni muundo wa serikali mbili, kama ulivyopendekezwa na Bunge Maalumu la Katiba. 16% pekee ya watanzania bara wanapendelea wazo la kuwa na muundo wa serikali tatu, kama ulivyopendekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Hata hivyo, takwimu hizi zinapaswa kuangaliwa kwa tahadhari, kwa kuwa hazihusishi maoni ya wazanzibari. Utafiti uliofanyika mwaka

2014 ulionesha kuwa uungaji mkono wa muundo wa serikali tatu miongoni mwa wazanzibari ulikuwa mkubwa, kwa asilimia 46.

Tukiangalia mbele, wananchi wapo wazi kwenye mambo mawili: wana hamu kubwa ya kupata katiba mpya na wangependa kuanza mchakato huo upya na tume mpya, pamoja na ukusanyaji upya wa maoni. Zaidi, endapo litatumika andiko la zamani kama sehemu ya kuanzia majadiliano, wananchi wangependa itumike rasimu iliyotolewa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba (rasimu ya Warioba).

Kwa kuweka haya yote pamoja, mchakato ujao wa kutengeneza katiba mpya nchini Tanzania utapaswa kutatua changamoto kuu tatu: (i) ufahamu na ushirikishwaji, (ii) uhalali miongoni mwa wanachi, na (iii) makubaliano ya maudhui ya katiba. Suala la kwanza ni rahisi zaidi kutekelezwa, kwa kutumia jitihada mbalimbali za kuwafahamisha wananchi hususani wanawake na makundi mengine yaliyoko pembezoni pamoja na kufanya jitihada mahususi za kuondoa changamoto ya usawa wa kijinsia. Suala la uhalali ni gumu, lakini linaweza kufanyiwa kazi kupitia aina ya uongozi ambayo itazuia mchakato wa katiba kuingia kwenye vita za ushabiki wa kisiasa na hivyo kutatua tofauti zinazojitokeza kupitia mijadala badala ya kutumia wingi wa idadi ya watu.

Kufikia makubaliano kwenye suala la maudhui ya katiba pengine ndiyo changamoto kubwa kuliko zote. Suala hili linahitaji usawa kamili katika kusikiliza maoni ya wananchi na wakati huo huo kutoa mwongozo wenye busara kwenye baadhi ya masuala mazito. Kuendeleza mchakato pale ulipokomea kuna hatari ya kurejesha vita vilivyokuwepo wakati wa awamu ya mwisho. Kwa kufuata mwongozo wa wananchi wa kuanza ukurasa upya na kuanza tena mchakato wa kukusanya maoni utasaidia kujenga uaminifu na kuondoa wasiwasi. Kutengeneza rasimu inayoendana na maoni ya wananchi kwenye suala la uwajibikaji ni rahisi, lakini suala la muungano ni gumu zaidi. Na linapaswa kujadiliwa kwa uangalifu mkubwa. Suala la kutumia idadi kubwa ya watu ambapo Tanzania bara itaizidi Zanzibari halifai na litaleta shida.

Nchi mbalimbali duniani huwawia vigumu kufikia muafaka kwenye suala linalofanana na hili la Tanzania – Scotland na Uingereza, Hong Kong na China, Puerto Rico na Marekani, ni mifano mitatu inayoendana. Kwa wazanzibari ambao hawapendezwi na hadhi ya Zanzibar inayoonekana kuwa ndogo kwenye muungano, kuondoa kipengele cha muundo wa serikali tatu kilichowekwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ni kama kuweka keki mezani na kisha kuwaambiwa watu wasile.

Fursa nzuri ya kutafuta suluhisho ni kwa kutatua changamoto mbili kubwa: ushirikishwaji na uhalali. Kwa kutumia mchakato ulio wazi, unaoshirikisha wananchi na kutatua tofauti zinazojitokeza kwa njia ya mazungumzo, tunaweza kabisa kufikia muafaka. Kwa kutumia mchakato wa wazi na uongozi jumuishi tutafanikiwa.